


JIMBO KATOLIKI IRINGA
TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI TOSAMAGANGA (TIHAS)



S.L.P 50 TOSAMAGANGA
IRINGA

SIMU: 0769 432 532 (MKUU WA TAASISI)/ 0762 482 704 (MHASIBU)

BARUA PEPE: tosamagangainstitute@gmail.com

TOVUTI: www.tihhas.ac.tz

UTANGULIZI

Tunashukuru kwa kuendelea kuwa mdau wa Elimu katika kada ya Afya kwa kupitia Taasisi yetu. Taasisi inakuarifu tarehe ya kufungua mwaka mpya wa masomo wa 2023/2024 kwa mkupuo wa mwezi wa tisa itakuwa ni tarehe **16/10/2023**. Taasisi yetu inatoa kozi mbili za afya ambazo ni Utabibu (Clinical Medicine) pamoja na Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifery) kwa hatua ya Astashahada na Stashahada.

YAH: ADA NA MALIPO MENGINE KWA MWAKA WA TATU (2023/2024) KWA KOZI YA UTABIBU (CLINICAL MEDICINE).

Na	AWAMU	ADA	MALAZI (Hostel)
1	Awamu ya kwanza (Wakati wa kuripoti muhula wa kwanza)	600,000	BURE
2	Awamu ya pili (01/01/2024)	500,000	BURE
3	Awamu ya tatu (Wakati wa kuripoti muhula wa pili)	600,000	BURE
4	Awamu ya nne (01/07/2024)	500,000	BURE
	JUMLA	2,200,000/=	BURE

NB

1. Gharama za Ada, Chakula na Malazi iliyoainishwa kwenye jedwali ilipwe kwenye Kumbukumbu namba ya malipo (**Control Number**) ya mwanachuo kupitia Benki ya CRDB.
2. Ada haitabadilika katikati/ndani ya mwaka wa masomo, lakini inaweza kubadilika mwanzo wa mwaka wa masomo unaofuata kutegemeana na mabadiliko ya uchumi wa Taasisi, Jimbo na Nchi.
3. Ada unaweza kulipa yote au kwa awamu nne kama ilivyoainisha kwenye jedwali
4. Mwanafunzi asipotimiza kulipa ada kwa awamu husika hatapokelewa au atarudishwa nyumbani na akikaa nyumbani kwa muda wa siku 21 na zaidi atapaswa kurudia mwaka.
5. Wale tu ambao wamelipa nusu ya ada ya muhula ndio watakaosajiliwa kwenye muhula husika.
6. Ada ikishalipwa hairudishwi.

GHARAMA YA MAZOEZI KWA VITENDO PAMOJA NA UTAFITI

Wanafunzi watafanya utafiti katika muhula wa kwanza ambapo gharama ya utafiti ni **Tsh. 100,000/=** na mazoezi kwa vitendo katika hospitali mbalimbali, mazoezi hayo yatafanyika katika hospitali zilizopo ndani ya wilaya ya Iringa Vijijini kwa muda wa wiki mbili, yaani siku kumi na nne (14). Gharama za mazoezi kwa vitendo ni **Tsh 50,000/=** mwanafunzi aje nayo mkononi wakati wa kuripoti. Lakini, katika kipindi hicho mwanafunzi atajitegemea gharama za usafiri kwenda kwenye vituo, chakula na malazi.

MICHANGO MINGINE

1. Gharama ya mitihani ya taifa ya Wizara ya Afya ni **Tshs.150,000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU wakati wa kuripoti.
2. Ada ya Udhhibiti Ubora (Quality Assurance Fee) Tshs.**15,000/=** Kwa ajili ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (**NACTVET**), UJE NA FEDHA TASILIMU wakati wa kuripoti.
3. Matibabu Tshs.**52,400/=** kwa asiye na bima na kwa mwenye bima afike na bima yake (UJE NA FEDHA MKONONI)
4. Mfuko wa serikali ya wanachuo ni **Tsh 10,000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU wakati wa kuripoti.
5. Gharama za marudio ya mtihani (supplementary exam) ni **Tsh. 50,000/=** kwa somo (kwa atakae shindwa fikia wastani) na maombi ya mtihani maalumu (Special sit exam) ni **Tsh. 50,000** kwa kila somo (kwa sababu maalum)
6. **MAHAFALI:** Gharama ya sherehe ya kuhitimu mwaka wa tatu ni **Tsh. 50,000/=** bila Joho (Vazi maalumu la sherehe ya kuhitimu.

Tunakutakia maandalizi mema na KARIBU.

ASANTE



ERICK L. MSEMWA

Mkuu wa Taasisi

